**NA. 06: TOLEO LA TAKWIMU ZA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII - ZANZIBAR KWA MWEZI WA JULAI - SEPTEMBA, 2025**

## 1.0 Utangulizi

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu wa utekelezaji wa majukumu yake iliyojipangia katika kuimarisha takwimu za Matukio ya Kijamii. Miongoni mwa takwimu hizo ni takwimu za Usajili wa Vizazi, Vifo, Ndoa na Talaka.

Toleo la robo ya tatu ya mwaka 2025 (Julai-Septemba), linatoa muhtasari wa takwimu za Matukio ya kijamii. Takwimu hizi zinatolewa kwa mlinganisho wa kijiografia (Wilaya) na kijinsia. Takwimu za Matukio ya Kijamii hutoa taarifa za idadi ya matukio ya kijamii yaliyosajiliwa na Wakala wa Usajili na Matukio ya Kijamii Zanzibar.

## 2.0 Lengo

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za Usajili wa Matukio ya Kijamii za ndani ya Zanzibar. Upatatikaji wa taarifa hizi ni muhimu katika kupanga maendeleo ya kijamii, kupima mafanikio ya Sera za Afya na kutambua changamoto za kijamii. Aidha, takwimu za matukio ya Kijamii husaidia katika kutathimini maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi, pia hutoa mwongozo muhimu kwa watafiti, serikali, na mashirika ya maendeleo katika kufanya tathimini na maamuzi sahihi kwa jamii. Toleo hili linawasilisha takwimu zifuatazo.

### 2.1 Usajili wa Vizazi Vilivyosajiliwa Ndani ya Wakati

Jumla ya Vizazi hai 8,179 vimeripotiwa kusajiliwa kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, 2025, ambapo 4,151 (50.8%) ni wanaume na wanawake 4,028 (49.2%), usajili unaonesha kuwa uwiano wa jinsi ni wanaume 103 kwa kila wanawake 100. Aidha, usajili umekuwa ukipanda na kushuka, ambapo mwezi wa Julai vizazi 2,419 (29.6%) vilisajiliwa na kuongezeka hadi vizazi 3,426 (41.9%) kwa mwezi wa Agost na kupungua hadi kufikia vizazi 2,334 (28.5%) (Jadweli Na. 1).

Kwa kipindi cha Julai - Septemba 2025 usajili unaonesha kuwa, Wilaya ya Mjini imeripotiwa kusajili vizazi hai vingi zaidi ambavyo ni 1,583 (19.4%) ikifuatia na wilaya ya Wete ambayo imeripotiwa kusajili vizazi 1,046 (12.8%), wilaya ya Kaskazini "B" imeripotiwa kusajili vizazi hai kidogo zaidi ambavyo ni 108 (1.3%) ukilinganisha na wilaya nyingine.

**Jadweli Na. 1: Usajili wa Vizazi hai kwa Jinsi na Wilaya, Julai-Sept 2025**

| Wilaya | Julai-2025 | | | Agost-2025 | | | Sept-2025 | | | Julai-Sept, 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 115 | 105 | **220** | 144 | 158 | **302** | 108 | 92 | **200** | 367 | 355 | **722** |
| Kaskazini B | 22 | 19 | **41** | 19 | 30 | **49** | 9 | 9 | **18** | 50 | 58 | **108** |
| Kati | 41 | 56 | **97** | 200 | 200 | **400** | 148 | 142 | **290** | 389 | 398 | **787** |
| Kusini | 32 | 31 | **63** | 82 | 68 | **150** | 41 | 45 | **86** | 155 | 144 | **299** |
| Mjini | 263 | 250 | **513** | 306 | 286 | **592** | 237 | 241 | **478** | 806 | 777 | **1,583** |
| Magharibi A | 136 | 132 | **268** | 228 | 229 | **457** | 96 | 115 | **211** | 460 | 476 | **936** |
| Magharibi B | 99 | 96 | **195** | 150 | 147 | **297** | 115 | 98 | **213** | 364 | 341 | **705** |
| Micheweni | 140 | 165 | **305** | 154 | 161 | **315** | 98 | 115 | **213** | 392 | 441 | **833** |
| Wete | 179 | 144 | **323** | 209 | 188 | **397** | 174 | 152 | **326** | 562 | 484 | **1,046** |
| Chakechake | 112 | 124 | **236** | 139 | 134 | **273** | 101 | 96 | **197** | 352 | 354 | **706** |
| Mkoan | 86 | 72 | **158** | 100 | 94 | **194** | 68 | 34 | **102** | 254 | 200 | **454** |
| **Jumla** | **1,225** | **1,194** | **2,419** | **1,731** | **1,695** | **3,426** | **1,195** | **1,139** | **2,334** | **4,151** | **4,028** | **8,179** |

### 2.1.1 Mlinganisho wa Usajili wa Vizazi Hai, April-Juni 2025 na Julai - Septemba 2025

Katika kipindi cha April – Juni 2025, usajili wa vizazi hai ulikuwa mkubwa (vizazi 10,062) kwa jumla ukilinganisha na kipindi cha Julai-Septemba 2025 (8,179). Adha, usajili unaonesha kuwa wanaume walikuwa 5,183 (51.5%) na wanawake 4,879 (48.5%). Wilaya ya Mjini ndiyo ilisajili vizazi vingi zaidi ambavyo ni 2,557 (25.4%), ikifuatiwa na Wilaya ya Wete 1,319 (13.1%) na Magharibi B 1,242 (12.3%) huku Wilaya ya Kaskazini B iliripotiwa kusajili idadi ndogo (chini ya vizazi 100 ambavyo ni 96 sawa na asilimia 1.0).

Kwa upande wa Julai - Septemba 2025, kuliripotiwa kupungua kwa usajili wa vizazi hai, ambapo jumla ya vizazi 8,179 vilisajiliwa, hii ni sawa na upungufu wa usajili wa vizazi 1,889 (18.8%) ikilinganishwa na robo mwaka ya April – Juni, 2025. Upungufu huo unaonekana kwa wilaya zote isipokuwa wilaya ya Kaskazini B ambayo inaongezeko la vizazi 12 (0.1%) na wilaya ya Kati 434 (5.3%). Kwa ujumla, tofauti kubwa kati ya vipindi hivi viwili inaashiria kutokuimarika kwa upatikanaji wa huduma za usajili wa vizazi hai. Hali hii inatoa ishara ya jamii kutokuhamasika katika usajili wa matukio ya kijamii, aidha kushuka kwa kiwango cha uzazi (Fertility rate) ndio kunapelekea kushuka kwa usajili wa matukio ya kijamii.

**Jadweli Na. 2: Mlinganisho wa Usajili wa Vizazi kwa Jinsi na Wilaya, April-Juni 2025 na Julai-Sept 2025**

| Wilaya | April-Juni, 2025 | | | Julai-Sept, 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 377 | 401 | **778** | 367 | 355 | **722** |
| Kaskazini B | 46 | 50 | **96** | 50 | 58 | **108** |
| Kati | 180 | 173 | **353** | 389 | 398 | **787** |
| Kusini | 187 | 191 | **378** | 155 | 144 | **299** |
| Mjini | 1,341 | 1,216 | **2,557** | 806 | 777 | **1,583** |
| Magharibi A | 552 | 506 | **1,058** | 460 | 476 | **936** |
| Magharibi B | 647 | 595 | **1,242** | 364 | 341 | **705** |
| Micheweni | 515 | 493 | **1,008** | 392 | 441 | **833** |
| Wete | 693 | 626 | **1,319** | 562 | 484 | **1,046** |
| Chakechake | 415 | 369 | **784** | 352 | 354 | **706** |
| Mkoani | 230 | 259 | **489** | 254 | 200 | **454** |
| **Jumla** | **5,183** | **4,879** | **10,062** | **4,151** | **4,028** | **8,179** |

**2.1.2 Mlinganisho wa Usajili wa Vizazi Hai, Julai – Sept, 2024 na Julai - Sept, 2025**

Jadweli Na. 3 linaonesha kuwa katika kipindi cha Julai - Septemba 2024, usajili wa vizazi hai ulikuwa wa kiwango cha (14,152) ukilinganisha na wa Julai - Septemba 2025 vizazi (8,179) sawa na upungufu wa usajili wa vizazi 5,973 (42.2%).

Upungufu huo unaonekana zaidi katika wilaya ya Mkoani (kutoka vizazi 2,330 kwa robo ya Julai - Septemba, 2024 hadi vizazi 454 kwa robo ya Julai – Septemba, 2025), ikifuatiwa na wilaya ya Kaskazini A (kutoka vizazi 1,895 kwa robo ya Julai - Septemba, 2024 hadi vizazi 722 kwa robo ya Julai – Septemba, 2025) na wilaya ya Chakechake usajili umepungua (kutoka vizazi 1,721 kwa robo ya Julai - Septemba, 2024 hadi vizazi 354 kwa robo ya Julai – Septemba, 2025).

Kupungua huku kwa usajili ya vizazi kwa robo mwaka ya Julai – Septemba, 2025 kunaashiria kukosekana kwa ushajihishajia endelevu kuhusu umuhimu wa usajili vizazi au jamii kukosa uelewa wa kusajili na hitilafu za mifumo ya kielektronik na changamoto za mitandao.

**Jadweli Na. 3: Mlinganisho wa Usajili wa Vizazi hai kwa Jinsi na Wilaya, Julai- Septemba, 2024 na Julai-Septemba, 2025**

| WILAYA | Julai-Sept, 2024 | | | Julai-Sept, 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 877 | 1,018 | **1,895** | 367 | 355 | **722** |
| Kaskazini B | 261 | 242 | **503** | 50 | 58 | **108** |
| Kati | 590 | 616 | **1,206** | 389 | 398 | **787** |
| Kusini | 220 | 247 | **467** | 155 | 144 | **299** |
| Mjini | 682 | 1,209 | **1,891** | 806 | 777 | **1,583** |
| Magharibi A | 122 | 138 | **260** | 460 | 476 | **936** |
| Magharibi B | 660 | 735 | **1,395** | 364 | 341 | **705** |
| Micheweni | 621 | 855 | **1,476** | 392 | 441 | **833** |
| Wete | 451 | 557 | **1,008** | 562 | 484 | **1,046** |
| Chakechake | 838 | 883 | 1,721 | 352 | 354 | 706 |
| Mkoani | 1,098 | 1,232 | **2,330** | 254 | 200 | **454** |
| Jumla | **6,420** | **7,732** | **14,152** | **4,151** | **4,028** | **8,179** |

## 2.2 Usajili wa Vifo

Jumla ya Vifo 463 vimesajiliwa kwa kipindi cha miezi mitatu (Julai – Septemba, 2025), ambapo wanaume walikuwa ni 299 ( 64.6%) na wanawake ni 164 (35.4%). hii inaonesha kuwa usajili wa vifo kwa wanaume ni mkubwa ukilinganisha na wanawake (Jadweli Na.4). Usajili wa vifo umekuwa ukiongezeka kila mwezi,mwezi wa Julai 2025 jumla ya vifo 134 (28.9%), vifo 157 (33.9%) mwezi Agosti 2025 na vifo 172 (37.2%) mwezi wa Septemba 2025.

Katika kipindi cha Julai – Septemba 2025, wilaya ya Mjini imesajili vifo 127 (27.4%), ikifuatiwa na wilaya ya Magharibi A iliyosajili vifo 57 (12.3%). Aidha, wilaya ya

Kaskazini “B” usajili wa vifo ni mdogo 9 (1.9%) kwa kipindi cha Julai – Septemba 2025 ukilinganishwa na wilaya nyingine (Jadweli 4).

**Jadweli Na. 4: Usajili wa Vifo kwa Jinsi na Wilaya, Julai-Sept 2025**

| Wilaya | Julai-2025 | | | Agost-2025 | | | Sept-2025 | | | Julai-Sept, 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 10 | 4 | **14** | 7 | 6 | **13** | 11 | 6 | **17** | 28 | 16 | **44** |
| Kaskazini B | 2 | 1 | **3** | 2 | 1 | **3** | 3 | - | **3** | 7 | 2 | **9** |
| Kati | 5 | 6 | **11** | 8 | 2 | **10** | 9 | 4 | **13** | 22 | 12 | **34** |
| Kusini | 5 | 1 | **6** | 4 | 3 | **7** | 4 | 2 | **6** | 13 | 6 | **19** |
| Mjini | 18 | 12 | **30** | 35 | 15 | **50** | 27 | 20 | **47** | 80 | 47 | **127** |
| Magharibi A | 6 | 6 | **12** | 9 | 4 | **13** | 21 | 11 | **32** | 36 | 21 | **57** |
| Magharibi B | 2 | 6 | **8** | 15 | 7 | **22** | 12 | 5 | **17** | 29 | 18 | **47** |
| Micheweni | 5 | 3 | **8** | 4 | 0 | **4** | 6 | 2 | **8** | 15 | 5 | **20** |
| Wete | 5 | 5 | **10** | 8 | 3 | **11** | 6 | 3 | **9** | 19 | 11 | **30** |
| Chakechake | 13 | 9 | **22** | 9 | 3 | **12** | 4 | 4 | **8** | 26 | 16 | **42** |
| Mkoani | 6 | 4 | **10** | 10 | 2 | **12** | 8 | 4 | **12** | 24 | 10 | **34** |
| Jumla | **77** | **57** | **134** | **111** | **46** | **157** | **111** | **61** | **172** | **299** | **164** | **463** |

### 2.2.1 Mlinganisho wa Usajili wa Vifo kwa Jinsi na Wilaya, April-Juni, 2025 na Julai-Septemba, 2025

Usajili wa vifo unaonekana kushuka kidogo kutoka 467 April-Juni 2025 hadi kufikia 463 July-Septemba 2025.

hii sawa na upungufu wa usajili wa vifo vinne (asilimia 0.9). Wilaya zinazoonesha upungufu zaidi wa usajili wa vifo, ni Wilaya ya Kati kutoka vifo 41 hadi vifo 34, Wilaya ya Kusini kutoka vifo 27 hadi vifo 19, Wilaya ya Micheweni kutoka vifo 24 hadi vifo 20, Chakechake kutoka vifo 46 hadi vifo 42 na Mkoani kutoka vifo 51 hadi vifo 34.

Aidha, kuliripotiwa ongezeko la usajili wa vifo kwa wilaya ya Kaskazini A (kutoka 35 hadi vifo 44), wilaya ya Kati (kutoka 126 hadi vifo 127), Magharibi A (kutoka 45 hadi vifo 57), Magharibi B (kutoka 34 hadi vifo 47) na Wete (kutoka 26 hadi vifo 30) kwa kipindi cha (April - Juni 2025) hadi (Julai-Septemba, 2025). Hali hii inawezekana kuwa inatokana na kuongezeka uelewa wa usajili wa vifo..

**Jadweli Na. 5: Mlinganisho wa Usajili wa Vifo kwa Jinsi April - Juni, 2025 na Julai – Sept 2025**

| Wilaya | April - Juni, 2025 | | | Julai – Sept 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 19 | 16 | **35** | 28 | 16 | **44** |
| Kaskazini B | 10 | 2 | **12** | 7 | 2 | **9** |
| Kati | 19 | 22 | **41** | 22 | 12 | **34** |
| Kusini | 18 | 9 | **27** | 13 | 6 | **19** |
| Mjini | 85 | 41 | **126** | 80 | 47 | **127** |
| Magharibi A | 28 | 17 | **45** | 36 | 21 | **57** |
| Magharibi B | 12 | 22 | **34** | 29 | 18 | **47** |
| Micheweni | 18 | 6 | **24** | 15 | 5 | **20** |
| Wete | 21 | 5 | **26** | 19 | 11 | **30** |
| Chakechake | 25 | 21 | **46** | 26 | 16 | **42** |
| Mkoani | 30 | 21 | **51** | 24 | 10 | **34** |
| **Jumla** | **285** | **182** | **467** | **299** | **164** | **463** |

### 2.2.2 Mlinganisho wa Usajili wa Vifo kwa Jinsi na Wilaya, Julai-Septemba, 2024 na Julai-Septemba, 2025

Jadweli Na. 6 linaonesha kuwa kiwango cha usajili kimeshuka kutoka usajili 1,120 Julai – Septemba 2024, wanaume wakiwa 623 na wanawake 497 hadi kufikia usajili 463 Julai - Septemba 2025 wanaume wakiwa 299 na wanawake 164

Upungufu huo zaidi umeonekana katika wilaya ya Mjini ambapo usajili umeshuka kutoka vifo 609 kwa Julai-Septemba, 2024 hadi vifo 127 kwa Julai - Septemba, 2025 ikifuatiwa na Wilaya ya Kaskazini A usajili umeshuka kutoka vifo 157 kwa Julai-Septemba, 2024 hadi vifo 44 kwa Julai - Septemba, 2025. Hali hii inaashiria kuimarika kwa huduma za afya na kupunguza idadi ya vifo..

**Jadweli Na. 6: Mlinganisho wa Usajili wa Vifo kwa Jinsi na Wilaya, Julai-Septemba, 2024 na Julai-Septemba, 2025**

| Wilaya | Julai – Sept 2024 | | | Julai - Sept, 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 64 | 93 | **157** | 28 | 16 | **44** |
| Kaskazini B | 17 | 5 | **22** | 7 | 2 | **9** |
| Kati | 13 | 6 | **19** | 22 | 12 | **34** |
| Kusini | 15 | 7 | **22** | 13 | 6 | **19** |
| Mjini | 327 | 282 | **609** | 80 | 47 | **127** |
| Magharibi A | 41 | 42 | **83** | 36 | 21 | **57** |
| Magharibi B | 44 | 31 | **75** | 29 | 18 | **47** |
| Micheweni | 29 | 11 | **40** | 15 | 5 | **20** |
| Wete | 40 | 8 | **48** | 19 | 11 | **30** |
| Chakechake | 10 | 7 | **17** | 26 | 16 | **42** |
| Mkoani | 23 | 5 | **28** | 24 | 10 | **34** |
| **Jumla** | **623** | **497** | **1,120** | **299** | **164** | **463** |

## 2.3 Usajili wa Ndoa

Jumla ya Ndoa 4,734 zimesajiliwa kwa kipindi cha Julai - Septemba, 2025. Jumla ya ndoa 2,321 (49.0%) zimesajiliwa mwezi wa Julai 2025, aidha, usajili umekuwa ukishuka kwa mwezi Agosti na Septemba kwa kusajilia ndoa 1,247 (26.3%) mwezi Agosti, 2025 na ndoa 1,166 (24.6%) kwa mwezi wa Septemba 2025 (Jadweli Na. 7).

Aidha, takwimu zinaonesha kuwa kwa kupindi cha Julai - Septemba 2025, wilaya ya Kati imesajili ndoa nyingi 1,215 (25.7%), ikifuatia na wilaya Magharibi B, Magharibi A na Mjini ambazo zimeripoti kusajili ndoa 989 (21.0%), 792 (16.7%) na 764 (16.1%) mtawalia. Aidha, wilaya ya Mkoani haikuripotiwa kusajili ndoa yoyote katika kipindi hicho, wakati wilaya ya Wete iliripotiwa kusajili ndoa 13 (0.3%) na wilaya ya Micheweni ndoa 41 (0.9%). Hii inatokana na mwamko mdogo wa jamii katika usajili wa ndoa ukilinganisha na ndoa zinazofungwa katika wilaya zote.

**Jadweli Na. 7: Usajili wa Ndoa kwa Wilaya, Julai – Septemba 2025**

| Wilaya | Julai-2025 | Agosti-2025 | Sept-2025 | Julai-Sept 2025 |
|---|---|---|---|---|
| Kaskazini A | 133 | 0 | 6 | **139** |
| Kaskazini B | 145 | 98 | 89 | **332** |
| Kati | 448 | 648 | 119 | **1,215** |
| Kusini | 194 | 30 | 90 | **314** |
| Mjini | 442 | 3 | 319 | **764** |
| Magharibi A | 400 | 193 | 199 | **792** |
| Magharibi B | 432 | 254 | 303 | **989** |
| Micheweni | 18 | 9 | 14 | **41** |
| Wete | 9 | 2 | 2 | **13** |
| Chakechake | 100 | 10 | 25 | **135** |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Jumla | **2,321** | **1,247** | **1,166** | **4,734** |

### 2.3.1 Mlinganisho wa Usajili wa Ndoa kwa April - Juni, 2025 na Julai – Sept 2025

Jadweli Na. 8 linaonesha kuwa usajili wa ndoa umeongezeka kutoka usajili wa ndoa 3,871 April-Juni na kuongezeka hadi kufikia ndoa 4,734 Julai- Sept 2025.

Aidha, takwimu zinaonesha kuwa wilaya ya Magharibi B inaongozakwa kuwa na usajili wa ndoa 2,124 kwa kipindi cha April-Septemba, ikifuatiwa na wilaya ya Mjini na Magharibi A ambazo zimesajili 1,668 na 1,612 mtawaliaya. Aidha, katika kipindi hicho wilaya ya Mkoani imesaliji ndoa mmoja tu.

**Jadweli Na. 8: Mlinganisho wa Usajili wa Ndoa kwa April - Juni, 2025 na Julai – Sept 2025**

| **Wilaya** | **April – Juni, 2025** | **Julai – Sept 2025** | **Tofauti** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| Kaskazini A | 262 | 139 | -123 | **401** |
| Kaskazini B | 150 | 332 | 182 | **482** |
| Kati | 147 | 1,215 | 1068 | **1,362** |
| Kusini | 185 | 314 | 129 | **499** |
| Mjini | 904 | 764 | -140 | **1,668** |
| Magharibi A | 820 | 792 | -28 | **1,612** |
| Magharibi B | 1,135 | 989 | -146 | **2,124** |
| Micheweni | 40 | 41 | 1 | **81** |
| Wete | 33 | 13 | -20 | **46** |
| Chakechake | 194 | 135 | -59 | **329** |
| Mkoani | 1 | 0 | -1 | **1** |
| **Jumla** | **3,871** | **4,734** | **863** | **8,605** |

## 2.4 Usajili wa Talaka

Jadweli Na. 9 linaonesha kuwa jumla ya Talaka 317 zimesajiliwa kwa kipindi cha Julai–Septemba, 2025. Aidha usajili ulikuwa na kupanda na kushuka, mwezi Julai jumla ya talaka 124 (39.1%) zimesajiliwa, mwezi Agosti na Septemba usaliji ulikuwa 83 (26.2%) na 110 (34.7%) mtawalia.

Aidha, Wilaya ya Magharibi "B"imeripoti kusajili idadi kubwa 126 (39.7%) ya talaka ikilinganishwa na wilaya nyingine kwa kipindi cha Julai-Septemba 2025, ikifuatiwa na Wilaya ya Magharibi A iliyoripotiwa kusajili talaka 50 (15.8%) na wilaya ya Kusini ilisajili talaka 47 (14.8%). Bado kuna mwamko mdogo wa usajili wa talaka kwa jamii, hali hii inaonekana kuwa kubwa zaidi katika wilaya ya Kaskazini B, Chakechake, na

Mkoani ambazo hazikuwa na usajili kabisa wa talaka kwa kipindi hicho.

**Jadweli Na. 9: Usajili wa Talaka kwa Mwezi, Julai - Septemba 2025**

| Wilaya | Julai-2025 | Agosti-2025 | Septemba-2025 | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Kaskazini A | 2 | 0 | 0 | 2 |
| Kaskazini B | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 14 | 18 | 14 | 46 |
| Kusini | 12 | 5 | 30 | 47 |
| Mjini | 28 | 0 | 15 | 43 |
| Magharibi A | 30 | 8 | 12 | 50 |
| Magharibi B | 38 | 51 | 37 | 126 |
| Micheweni | 0 | 1 | 1 | 2 |
| Wete | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Chakechake | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Jumla | **124** | **83** | **110** | 317 |

### 2.4.1 Mlinganisho wa Usajili wa Talaka kwa April - Juni, 2025 na Julai – Sept 2025

Jumla ya talaka 691 zimesajiliwa kwa miezi yote sita (April –Septemba, 2025) kati ya hizo talaka 374 (54.1%) zilisajiliwa April hadi Juni, 2025 na talaka 317 (45.9%) Julai hadi Septemba 2025, hii inaonesha upungufu wa jumla ya talaka 57 (-15.2%) ikilinganishwa na robo pili (Jadweli Na. 10).

Aidha, takwimu zinaonesha kuwa wilaya ya Magharibi B inaongoza kwa usajili kutoka talaka 119 hadi 126 kwa kipindi cha April – Juni 2025 na July-Septemba 2025 sawa na ongezeko la asilimia 6. Aidha usajili unaonekana kuongezeka katika wilaya za Magharibi A, Kusini, Micheweni na wilaya ya wete. Jadweli Na. 10. Usajili wa talaka unaonekana kushuka katika wilaya za Chakechake, Kaskazini A, Kaskazini B, Wilaya ya Kati, na Mjini hii inatokana na uwelewa mdogo wa usajili wa talaka au kutokuwa.

**Jadweli Na. 10: Mlinganisho wa Usajili wa Talaka kwa April - Juni, 2025 na Julai – Septemba 2025**

| **Wilaya** | **Usajili wa Talaka kwa Mwezi April hadi Septemba 2025** | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **April – Juni, 2025** | **Julai – Sept 2025** | **Tofauti** | **Jumla** |
| Kaskazini A | 29 | 2 | -27 | **31** |
| Kaskazini B | 6 | 0 | -6 | **6** |
| Kati | 58 | 46 | -12 | **104** |
| Kusini | 22 | 47 | 25 | **69** |
| Mjini | 68 | 43 | -25 | **111** |
| Magharibi A | 20 | 50 | 30 | **70** |
| Magharibi B | 119 | 126 | 7 | **245** |
| Micheweni | 0 | 2 | 2 | **2** |
| Wete | 0 | 1 | 1 | **1** |
| Chakechake | 52 | 0 | -52 | **52** |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **Jumla** | **374** | **317** | **-57** | **691** |

### 2.4.2 Uhusiano na Mwenendo wa Ndoa na Talaka

Wakati usajili wa ndoa umeongezeka kutoka 3,871 kwa robo ya April – Juni, 2025 hadi ndoa 4,734 kwa robo ya Julai – Septemba, 2025, idadi ya talaka imepungua kutoka 374 kwa robo ya April – Juni, 2025 hadi talaka 317 kwa robo ya Julai – Septemba, 2025. Hii inaweza kuashiria uimarishaji wa uhusiano ya wanandoa au kupungua athari za mizozo, ambayo inaweza kuwa usuluhishi na elimu ya ndoa inayotolewa kupitia viongozi wa dini.

## 3.0 Hitimisho

Kwa ujumla, taarifa za matukio ya kijamii ni muhimu sana kwa kuimarisha huduma za kijamii, kuleta mabadiliko chanya, na kukuza ustawi wa jamii. Jamii inapaswa kushiriki kikamilifu katika kusajili matukio ya kijamii kwa maendeleo ya Taifa.

Ikumbukwe kuwa takwimu zilizowasilishwa hapa ni zile tu zilizosajiliwa rasmi kupitia Ofisi za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA). Kuna matukio mengi kwenye jamii hasa ya vifo na talaka ambayo yanatokea katika jamii na hayasajiliwi rasmi. Aidha, jamii inasisitizwa kuwa na utamaduni wa kusajili matukio ya Kijamii kwa mamlaka husika ili yaweze kusajiliwa, na kuisaidia serikali na wadau wengine wa maendeleo katika kupanga mipango yenye tija kwa taifa.

## Maelezo Muhimu

- Kizazi hai ni tukio la mtoto kuzaliwa akiwa hai, yaani, mtoto ambaye amezaliwa ana pumzi, anafanya harakati, na ana ishara za maisha. Kizazi hai mara nyingi hufuatana na mchakato wa kawaida wa kujifungua, ambapo mtoto huzaliwa kuja ulimwenguni.

- Kifo ni tukio la mwisho la kuishi. Ni tukio ambalo mwili huacha kabisa kufanya kazi kwa binadamu, kifo hutokea wakati moyo unasimama na kusitisha mtiririko wa damu mwilini, na ubongo kusimama kufanya kazi.

- Sheria Namba 3 ya 2018, inaeleza kuwa Ofisi za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA) ina majukumu ya kusajili Matukio ya kijamii na kutoa vyeti maalum, matukio hayo ni Vizazi, Vifo, Ndoa, Talaka na Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi na Wasiokua Wazanzibari Wakaazi.

- Sheria Namba 9 ya mwaka 2007 inaeleza kuwa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar ina mamlaka ya kuratibu na kusimamia uendeshaji wa kazi za takwimu katika taasisi zote za Serikali na binafsi zinazofanya shughuli zake hapa Zanzibar.

*Kwa Ufafanuzi Zaidi Tafadhali Wasiliana na:*


**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI,**
S.L.P 2321, 7 Barabara ya Fumba, 71125 Mjini Magharibi,
Zanzibar – Tanzania.
Simu +255 24 2231869
Faksi: +255 24 2231742
Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz
Website: www.ocgs.go.tz

**WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMI**
Simu: +255 772 400 597
S.L.P: 264
Barua pepe: info@zcsra.go.tz
Flamingo, Migombani Zanzibar Tanzania.